**CHUO CHA ELIMU YA BIASHARA (CBE)**

**DAR ES SALAAM/ DODOMA/ MWANZA/ MBEYA**

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MALALAMIKO YA WANAFUNZI WA '*MARCH INTAKE*' 2025/2026 – CBE KAMPASI YA MWANZA**

**TAREHE: 09/08/2026**

Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) kimepokea na kufuatilia malalamiko ya baadhi ya wanafunzi wa Dirisha la Machi 2025/2026 wa CBE Kampasi ya Mwanza kuhusu kuchelewa kwa matokeo yao kupandishwa katika mfumo wa Baraza la Taifa la Elimu na Mafunzo ya Ufundi (NACTVET), hali ambayo imeathiri taratibu zao za kuendelea na masomo ya ngazi za juu na fursa nyingine zinazohitaji matokeo hayo.


Suala hili linawahusu wanafunzi wawili (2) wa programu ya NTA Level 5 katika Diploma in Procurement and Supplies Management (DPS) ambao wanakabiliwa na changamoto ya kutofautiana kwa taarifa zilizopo katika mfumo wa NACTVET na taarifa zilizopo CBE hivyo kusababisha kuchelewa kwa matokeo yao kupandishwa katika mfumo wa NACTVET.

Katika mwaka wa masomo 2025/2026 jumla ya wanafunzi 41 walistahili kupandishiwa matokea yao katika mfumo wa NACTVET, ambapo wanafunzi 23 matokeo yao ya NTA Level 5 na 6 yamepandishwa kikamili kwa ajili ya kuendelea na maombi ya hatua za juu za kitaaluma na wanafunzi 16 matokeo yao hajakamilika kwasababu wanapaswa kurudia baadhi ya mitihani.

CBE inapenda kuwataarifu wanafunzi husika na umma kwa ujumla kuwa kwa kushirikiana na NACTVET Kanda ya Ziwa, imechukua hatua za kina na za haraka kufuatilia na kulifanyia kazi suala la wanafunzi hawa katika kurekebisha taarifa hizo ili kuwezesha mchakato wa matokeo kukamilika.

CBE inawahakikishia wanafunzi husika kuwa matokeo yao hayatapotea wala kucheleweshwa kwa sababu ya changamoto hii, na hatua zinazohitajika zinaendelea kuchukuliwa ili kuwawezesha kuendelea na hatua zao za kitaaluma, ikiwemo kuomba kujiunga na programu za shahada.

Aidha, Chuo kinawahakikishia wanafunzi na umma kwa ujumla kuwa suala hili linaendelea kufanyiwa kazi kwa haraka, na Uongozi wa Chuo utaendelea kutoa taarifa rasmi kuhusu hatua zitakazochukuliwa kadri mchakato unavyoendelea.



**Georgina Addo Misama**

**Kaimu Mkuu wa Kitengo Mawasiliano na Masoko**
**Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE)**